# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 26 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) APRILI 2023

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# NI MUHIMU MKANDARASI SUMA JKT KWA KUZINGATIA MKATABA KUONGEZA NGUVU KATIKA UJENZI WA OFISI ZA TSC

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliingia Mkataba na Mkandarasi SUMA JKT Construction Ltd kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Tume unaotekelezwa katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma.

Mradi huo unaogharimu kiasi cha shilingi 6,499,982,353.03 ambao unatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18 umeanza Desemba 6, 2022 na utakamilika ifikapo Juni 5, 2024. TSC tayari imelipa kiasi cha shilingi 500,000,000 ikiwa ni malipo ya wali ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Hivi karibuni na kwa nyakati tofauti viongozi mbalimbali akiwemo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, Naibu Waziri OR –TAMISEMI, Mhe. Deogratius Ndejembi, Wajumbe wa Tume, Menejimenti ya TSC, Baraza la Wafanyakazi TSC, Kamati ya Ukaguzi ya TSC pamoja na viongozi wengine wamefanya ziara kwenye eneo hilo kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi.

Pamoja na kwamba mradi huo unakwenda vizuri, ilibainika kuwa bado uko nyuma ikilinganishwa na mpango kazi wa utekelezaji wake. Kwa mujibu wa maelezo ya mkandarasi, sababu iliyofanya utekelezaji kuwa nyuma ni kukutana na changamoto ya uwepo wa miamba migumu wakati wa uchimbaji wa msingi tofauti na ilivyotarajiwa.

Pamoja na sababu hiyo, viongozi hao kwa nyakati tofauti wamemwelekeza mkandarasi kuhakikisha maradi unakamilika kwa wakati uliopangwa, hivyo wamemshauri kuongeza nguvukazi ili kuharakisha utekelezaji.

Itakumbukwa kuwa kukamilika kwa mradi huu kutaleta ahueni kubwa kwa TSC ambayo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya ofisi kwa ajili ya watumishi pamoja na nvya kuhifadhi nyaraka. Hivyo, ni imani yetu kuwa Mkandarasi, SUMA JKT atatekeleza kwa kuzingatia mkataba ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama


**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania   tumeyautumishiwawalimutanzania

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015. TSC ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma, Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, miongoni mwa majukumu ya TSC ni kusimamia masuala yanayohusu ajira ya Mwalimu ambayo ni kusajili na kutoa barua za ajira rasmi; kuthibitisha kazini; kupandisha vyeo; kubadilisha kazi/cheo waliojiendeleza; kuandaa Tange, kupitisha na kuratibu maombi ya kuajiriwa upya kwenye Utumishi wa Umma.

TSC pia inawajibika kushughulikia mafao ya wastaafu na mirathi ambayo haishughulikiwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kukokotoa mafao na kuwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hazina kwa ajili ya uhakiki na malipo.

Jukumu lingine ni kusimamia Maadili na Nidhamu kwa Walimu kwa kuwaelimisha na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanaokiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Sheria hiyo pia imeipa TSC jukumu la kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa katika upangaji wa walimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule pamoja na kusimamia Programu za Mafunzo ya Walimu Kazini.

Majukumu mengine yanayotekelezwa na ofisi hiyo ni kufanya tafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Utumishi wa Walimu pamoja na kufanya tathmini ya hali ya walimu na



*Moja ya Mafunzo ya Kamati za Wilaya yakiwa yanaendelea.*

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI




*Baadhi ya pikipiki zilizonunuliwa chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.*

kumshauri Waziri anayehusika na mafunzo ya walimu kuhusu idadi, aina ya mafunzo na uhitaji wa walimu nchini.

TSC inatekeleza majukumu haya kupitia Ofisi yake ya Makao Makuu iliyopo mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma pamoja na ofisi 139 zilizopo katika kila Wilaya Tanzania Bara na inasimamia walimu 258,291 ambao kati yao Walimu 173,591 ni wa Shule za Msingi na Walimu 84,700 ni wa Shule za Sekondari.

Katika kipindi cha miaka miwili tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani baada ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mhe. John Joseph Pombe Magufuli kufariki dunia akiwa madarakani Machi 17, 2021, TSC imeendelea kupata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa kutoa huduma kwa walimu.

Walimu 24,343 waliajiriwa na kusajiliwa, 14,799 walithibitishwa kazini, Walimu 161,432 walipandishwa vyeo, 20,032 walibadilishiwa miundo baada ya kujiendeleza na Walimu 6,436 walipewa vibali vya kustaafu. Pia, Walimu 272 waliomba kuajiriwa upya katika Utumishi wa Umma na maombi yao kufanyiwa kazi na kuwasilishwa OR – UTUMISHI kwa hatua zaidi.

Ndani ya miaka miwili ya Rais Samia madarakani, TSC kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) ilifanya kazi ya kukusanya, kuchambua na kuandaa taarifa ya tathimini ya usambazaji na uwiano wa walimu kupitia mfumo wa School Information System (SIS).

Katika kipindi cha miaka miwili jumla ya majalada 466 ya pensheni, mirathi na mikataba yalipokelewa. Majalada hayo, yalifanyiwa uchambuzi wa nyaraka na ukokotoaji wa hesabu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hazina kwa ajili ya malipo. Kati ya majalada hayo, 191 yalihusu mikataba, 70 ya pensheni na 205 yalihusu mirathi. Majalada



*Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (wa tatu kutoka kulia) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Januari 24, 2023 mjini Morogoro.*

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

301 yaliyosalia yanaendelea kushughulikiwa kwa kadri idara inavyopokea vielelezo muhimu kutoka kwa waajiri/walimu au wasimamizi wa mirathi.

Rais Samia pia ameiwezesha TSC Mfumo wa Kielektroniki wa Teacher's Service Management Information System (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma kwa walimu. Mfumo huo umezinduliwa rasmi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Agellah Jasmine Kairuki Machi 16, 2023 tayari kwa matumizi ambapo Mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi kuhusu namna ya kutumia mfumo huo yanaendelea kutolewa.

Mafunzo yaliyokwisha kufanyika yalihusisha watumishi kutoka mikoa kumi na miwili ambayo ni Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Dodoma, Pwani, Tanga, Rukwa, Katavi, Kigoma, Mara, Simiyu na Singida. Mafunzo hayo pia yalihusisha baadhi ya wakuu wa shule kutoka Shule za Msingi na Sekondari za jijini Dodoma, Maafisa saba (7) kutoka TSC Makao Makuu pamoja na Wilaya ya Morogoro na Kishapu.

Mfumo huo utarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ikiwa ni pamoja na kushughulikia Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, Malalamiko, Mafao ya Ajira ya Mkataba na Mirathi na Pensheni ya kabla ya tarehe 1 Julai, 2004, Usajili wa Walimu na kutunza taarifa za wageni.

Sambamba na hayo, Rais Samia ameiwezesha TSC kufanya jumla ya mikutano ya Tume kumi (10) kati ya kumi (10) iliyopangwa; Kamati za Wilaya 139 zilifanya vikao vya kisheria 1,063 kati ya vikao 1,390 vilivyopaswa kufanyika kwa mujibu wa Sheria; jumla ya wateja 10,682 walifika ofisini na kupata huduma zihusuzo masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu yakiwemo ajira, mirathi, mikataba, mashauri ya nidahamu na mafao.

Aidha, jumla ya malalamiko 5,440 yalipokelewa na kushughulikiwa. Malalamiko hayo yalihusu kupandishwa vyeo, kubadilishiwa cheo, kuthibitishwa kazini, mashauri ya nidhamu na masuala ya mafao. Tume iliratibu kikao cha Wadau (OR – Ikulu, OR – UTUMISHI, OR – TAMISEMI, CAG, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Elimu na PSSSF) kujadili changamoto mbalimbali kuhusu Utumishi wa Walimu na kutafuta ufumbuzi wa pamoja kama Serikali;

Pamoja na hayo, Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kushirikiana na Mradi wa World Vision Tanzania (WVT) waliandaa kitini kitakachotumika kufundishia Wakufunzi ngazi ya Wilaya kwenye maeneo ambako WVT wanaendesha shughuli zao. Kitini hicho kina mada mbalimbali zinazohusu Ajira, Maadili na Maendeleo ya Mwalimu. Kwa kuanzia, kwa kutumia kitini hiki mafunzo yametolewa kwa wakufunzi (TOT) kwenye ngazi ya Wilaya katika Mikoa ya Shinyanga (washiriki 48, kutoka Wilaya 6) na Iringa (washiriki 19 kutoka Wilaya 2).

Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 Tume ilikuwa imepokea jumla ya rufaa 341 ambapo kati ya hizo, rufaa 328 ziliwasilishwa katika mikutano ya Tume, zikajadiliwa na kutolewa uamuzi. Tume ilipokea jumla ya nakala za rufaa 78 zilizokatwa kwa Rais. Kati ya rufaa hizo mwenendo wa rufaa na vielelezo vya rufaa 72 zimetumwa kwa Rais na rufaa sita (6) zipo kwenye hatua ya kuandaliwa taarifa na mwenendo.



*Mwonekano wa hatua iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu unaofanyika katika eneo la Ndejengwa jijini Dodoma.*

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

Jumla ya Wachambuzi wa rufaa 15 na Wajumbe saba (7) wa Kamati ya kupitia Rufaa walijengewa uwezo kuhusu uchambuzi wa rufaa zinazowasilishwa Tume dhidi ya uamuzi wa Mamlaka za Nidhamu na zinazokatwa kwa Rais dhidi ya uamuzi wa Tume. Mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati ngazi ya Wilaya yalifanyika kikanda kwa Wilaya zote 139.

Katika usimamizi wa maadili ya walimu nchini, Walimu 3,226 walifunguliwa mashauri ya nidhamu ambapo utoro (1,936), kughushi vyeti (646) mahusiano ya kimapenzi (296), ulevi (120), ubadhirifu (16) na ukaidi (212). Kati ya Mashauri hayo, Mashauri 2,916 yalitolewa uamuzi na 310 yapo katika hatua mbalimbali za kufanyiwa kazi ili kuhitimishwa.

Chini ya usimamizi na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, TSC imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kuwasidia Wakuu wa Shule kwa nafasi zao za Mamlaka za Nidhamu ngazi ya Shule kumesaidia kushughulikia masuala ya walimu ngazi ya shule na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa walimu. Mwongozo huo umesambazwa kwa Wakuu wote wa Shule za Msingi na Sekondari.

Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuiwekea TSC mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa kuiwezesha kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu. Tume iliingia Mkataba na Mkandarasi SUMA JKT Construction Ltd kwa ajili ya usanifu na ujenzi (design and Build). Mkataba huu ni wa miezi 18 ambapo unategemea kukamilika Mwezi Juni, 2024. Mkandarasi yupo eneo la ujenzi na kazi inaendelea.

Ukweli ni kwamba hatuwezi kuainisha mafanikio yote ya TSC yaliyotokana na uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan lakini jambo lingine ambalo litaendelea kukumbukwa ni kuiwezesha TSC kufanya utafiti kuhusu kujitathmini iwapo imeweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448. Utafiti huo ulifanyika ambapo jumla ya wahojiwa 788 walihojiwa wakijumuisha walimu, Maofisa Elimu, Wananchi, Asasi za Kiraia, Waandishi wa Habari, Wabunge, Maofisa kutoka Wizara ya Elimu na OR - TAMISEMI.

Utafiti huo ulifanyika kwenye Wilaya 22 katika Mikoa saba (7) ya Tanzania Bara. Taarifa ya Utafiti huo inaonesha kuwa kati ya majukumu kumi na moja (11) ambayo Tume ilikabidhiwa kwa mujibu wa Sheria Sura 448, yapo majukumu ambayo Tume imeyatekeleza kwa asilimia zaidi ya 50.

Rais Samia ameiweka TSC kuwa miongoni mwa watekelezaji wa shughuli za mradi wa BOOST katika kipengele cha Shule salama na usimamizi wa Walimu. Kupitia mradi huo Tume imepangiwa kupata kiasi cha




*Mafunzo ya kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Tueme ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) yakiendelea.*

# TSC YAPATA MAFANIKIO LUKUKI, MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

shilingi 3,416,853,760.00 kutoka OR – TAMISEMI kwa mwaka wa kwanza (2022/2023) wa utekelezaji wa mradi ili kutekeleza kazi mbalimbali.

Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo ni kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, kuwajengea watumishi wa Tume uwezo katika kutekeleza majukumu ya Tume kwa kununua magari 15, laptops 159 na vifaa vingine vya TEHAMA na samani za ofisi na kufanya mapitio na kuhuisha Sheria na Kanuni zinazosimamia Utumishi wa Mwalimu kwa ajili ya kuandaa Sera ya Kitaifa ya Mwalimu.

Hadi Mwezi Machi, 2023 Tume imepokea kiasi cha shilingi 633,002,856.00 na katika fedha hizo, shilingi 353,126,400.00 zimetumika kwa ajili ya kazi zifuatazo; kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, kuwajengea uwezo Makatibu wasaidizi 139 wa Wilaya juu ya ufafanuzi huo, kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni zinazosimamia Utumishi wa Mwalimu kwa ajili ya kuandaa Sera ya Kitaifa ya Mwalimu ambapo taarifa imeandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwa wadau, Mchakato wa ununuzi wa magari 16, Laptop 159 na vifaa vingine vya TEHAMA na samani unaendelea.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Jamsine Kairuki (kushoto) akikabidhi tuzo maalum kwa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama kwa kufanikisha uundwaji wa Mfumo wa Kielektoniki wa Tume (TSCMIS).*

Rais Samia ameiwezesha TSC kununua pikipiki 74 kwa ajili ya ofisi za Wilaya. Pikipiki hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kuwafikia walimu na kutatua changamoto mbalimbali kwa wakati.

TSC imedhamiria kutoa huduma bora ili walimu waweze kutimiza wajibu wao wa kuwafundisha wanafunzi kikamilifu, hivyo itaendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuhakikisha huduma zinawafikia walimu kwa haraka zaidi.

Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha uongozi wake kwa kushughulikia malamiko mbalimbali ya walimu, moja ya malamiko makubwa ilikuwa ni kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, vilevile Rais Samia ameboresha mazingira ya kufundishia kwa kuongeza vyumba vya madarasa, ununuzi wa vitabu, ujenzi wa maabara pamoja na ukarabati na ujenzi wa shule.

Kutokana na juhudi hizo, walimu wana wajibu wa kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa kutanguliza maslahi ya watumishi wa umma. Hivyo ni vyema watumishi wa umma kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, weledi na nidhamu ili Tanzania iendelee kuwa na ustawi bora zaidi.

Hongera sana Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Walimu wana imani kubwa na wewe na wataendelea kukuunga mkono, kazi iendelee.


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
Hongera
Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Kwa
MIAKA MIWILI YA
UONGOZI SHUPAVU
"Mwenyekiti, Makamishna, Menejimenti na Watumishi wote wa TSC tunampongeza Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa Kutimiza Miaka Miwili ya Uongozi Shupavu.
#Kazi Iendelee
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
MIAKA MIWILI YA
UONGOZI SHUPAVU
Wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Machi 19, 2021 - Machi, 19, 2021
#Sekta ya Elimu
Bajeti ya Tume imeendelea kuongezeka mfululizo kutoka shilingi bilioni 14.773 hadi shilingi bilioni 15.654 kwa kipindi cha miaka hii miwili, ongezeko hili limeendelea kuongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu na hasa katika kutoa huduma kwa Walimu..
Shilingi milioni 175 zimetumika kuwajengea uwezo Watumishi 58 wa Tume kwa kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi lengo likiwa ni kuiwezesha Tume kuwahudumia Walimu kwa weledi na kuleta ufanisi zaidi.
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
MIAKA MIWILI YA
UONGOZI SHUPAVU
wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Machi 19, 2021 - Machi 19, 2023
#Sekta ya Elimu
Walimu ambao ni zaidi ya asilimia 50 ya Watumishi wote wa Umma pia wamenufaika na punguzo la Kodi katika Mishahara yao kutoka asilimia tisa (9) hadi asilimia nane (8) na hivyo kupunguza mzigo wa kodi kwa Walimu.
VAT
Walimu wamenufaika na kupungua kwa Tozo ya Thamani ya Elimu ya Juu
NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Walimu wamenufaika na kuongezeka kwa ukomo wa umri wa wategemezi wanaonufaika na Bima kutoka umri wa miaka 18 hadi 21.
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)
MIAKA MIWILI YA
UONGOZI SHUPAVU
Wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Machi 19, 2021 - Machi 19, 2023
#Sekta ya Elimu
Jumla ya Walimu 16,749 wameajiriwa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo Walimu walioko kazini kuhusu Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi wa Utumishi wa Walimu kulikoendana na kuandaliwa kwa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni hizo ili kuongeza urahisi wa uelewa wa Kanuni na kuwaepusha Walimu kujiingiza katika Makosa ya Kinidhamu.
Jumla ya Walimu 161,458 na Watumishi wa Tume 436 wanaowahudumia walimu wamepandishwa vyeo katika Kipindi hiki cha Miaka Miwili ya Uongozi wa Mama Daktari Samia Suluhu Hassan
Ujenzi wa Jengo la Ofisi la Makao Makuu ya Tume katika eneo la Njedengwa – Jijini Dodoma wenye thamani ya shilingi bilioni 6.6 unaoendelea chini ya Mkandarasi SUMA-JKT na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2024.
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
MIAKA MIWILI YA UONGOZI SHUPAVU
Wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Machi 19, 2021 - Machi 19, 2023
#Sekta ya Elimu
Mfumo mpya wa TEHAMA ujulikanao kama 'Teachers Service Commission Management Information System - TSCMIS' umejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha kazi ya kushughulikia Utumishi wa Walimu ikiwemo: Ajira za Walimu, Kuthibitisha Walimu Kazini, Kupandisha Walimu Vyeo, Kubadilisha Walimu Vyeo, Kushughulikia Mashauri ya Nidhamu ya Walimu na Maendeleo ya Walimu.
Katika kuboresha na kurahisisha zaidi hali ya utoaji huduma kwa Walimu nchini; Serikali imenunua na kuzipatia Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya na Makao Makuu Magari 17, Pikipiki 81 na hivi sasa inanunua Pikipiki nyingine 62, Kompyuta Mpakato (Laptops) 159, na vifaa vingine, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 3.38
Ujenzi na uzinduzi wa tovuti mpya ya Tume inayohudumia Watanzania zaidi ya milioni 61 (Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022) tofauti na ile ya awali iliyokua na changamoto kadhaa na kuhudumia wadau wachache zaidi ya idadi hiyo.
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
MIAKA MIWILI YA UONGOZI SHUPAVU
Wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Machi 19, 2021 - Machi, 19, 2023
#Sekta ya Elimu
Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya zote 139 yamefanyika kuwajengea uwezo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma ambapo pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yalijikita zaidi katika kuwaelimisha kuhusu taratibu bora za uendeshaji wa mashauri nidhamu kwa Walimu.
Mwongozo wa kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu katika kusimamia nidhamu ngazi ya shule uliandaliwa na kusambazwa katika shule zote za Umma nchini ili kuimarisha zaidi usimamizi wa maadili
Tume Utumishi wa Walimu Tanzania
www.tsc.go.tz

# WAZIRI KAIRUKI ASISITIZA WALIMU KUTHAMINIWA NA KUPATIWA MASLAHI YAO KWA WAKATI



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa pili wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa mwaka 2022/23 na Uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa Tume (TSCMIS). Uzinduzi huo umefanyika Machi 16,2023 katika Ukumbi wa Matokeo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jamsine Kairuki amesisitiza kuwa walimu wanapaswa kuthaminiwa, kuheshimiwa na kupatiwa maslahi yao kwa wakati ili waendelee kufundisha wanafunzi kwa bidii, weledi na uzalendo kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta ya elimu.

Waziri Kairuki ameyasema hayo wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) pamoja na kuzindua mfumo wa kielektroniki wa Tume hiyo (TSCMIS) Machi 16, 2023 katika Ukumbi wa Jengo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.

Waziri huyo amesema kuwa TSC ina wajibu mkubwa kuhakikisha maslahi na utu wa mwalimu unalindwa kwa nguvu zote pamoja na kutoa hamasa ili walimu waendelee kuwa na morali wa kutekeleza majukumu yao.

"Ni wajibu wenu kuhakikisha kuwa maslahi ya mwalimu na hadhi yake inalindwa kwa nguvu zote. Tambueni kuwa mnao wajibu mkubwa katika kuwafanya walimu wetu waweze kuleta mabadiliko ya elimu bora nchini kwa kuwahamasisha kutimiza wajibu wao na kulinda maslahi yao pamoja na kuwaondolea kero na malalamiko yaliyo ndani ya uwezo wenu," amesema Waziri Kairuki.



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Lazaro Komba akitoa neno la kumkaribisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Jamsine Kairuki ili afungue Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la (TSC) kwa mwaka 2022/23 na Uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa Tume (TSCMIS), Machi 16, 2023 katika Ukumbi wa Matokeo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*

# WAZIRI KAIRUKI ASISITIZA WALIMU KUTHAMINIWA NA KUPATIWA MASLAHI YAO KWA WAKATI

Pia, Waziri huyo amewataka watumishi wa Tume hiyo waliopo katika ngazi ya Wilaya kushirikiana na Maafisa elimu wa halmashauri na wathibiti ubora wa elimu katika kuhudumia na kuhamasisha walimu kutimiza wajibu wao.

Kiongozi huyo ameogeza kuwa Watumishi wa Tume hiyo hawapaswi kukaa ofisini kuwasubiri walimu badala yake wafanye ziara shuleni mara kwa mara ili kusikiliza kero na malamiko ya walimu na kutafuta ufumbuzi kwa wakati pamoja na kuendelea kutoa elimu juu ya Sheria, Kanununi na Maadili ya kazi hiyo.

Pamoja na hayo, Waziri Kairuki ameipongeza TSC kwa kufanya kazi kwa bidii katika kuhakikisha walimu wanapata maslahi yao pamoja na kuwasaidia kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia



*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Paulina Mkwama akizungumza wakati wa ufunguzi huo wa Baraza Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

miiko ya kazi hiyo kitu ambacho kimesaidia kupungua kwa malalamiko pamoja na kuimarika kwa nidhamu ya walimu.

Waziri ameongeza kuwa amefanya ziara na kuongea na walimu katika maeneo mbalimbali ambapo miongoni mwa malalamiko yaliyowasilishwa kwake ni baadhi ya walimu kucheleweshwa kubadilishiwa Muundo wa Utumishi, kutopandishwa madaraja/cheo kwa wakati na kupandishwa daraja la aina moja (kujirudia).

Alisema baada ya kupokea madai hayo aliiagiza TSC kufanya uchambuzi wa kina na kuwasilisha kwake malalamiko



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Jasmine Kairuki akibonyeza kitufe kuzindua Mfumo wa Kielektoniki wa Tume (TSCMIS). Uzinduzi huo umefanyika leo Machi 16,2023 katika Ukumbi wa Matokeo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Jasmine Kairuki (kushoto) akikabidhi tuzo maalum kwa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama kwa kufanikisha uundwaji wa Mfumo wa Kielektoniki wa Tume (TSCMIS).*

# WAZIRI KAIRUKI ASISITIZA WALIMU KUTHAMINIWA NA KUPATIWA MASLAHI YAO KWA WAKATI

ya walimu wote yanayohusiana na masuala ya maendeleo ya utumishi wao ambapo alipokea taarifa hiyo ambayo inaendelea kufanyiwa kazi ili kuona namna ya kuondoa changamoto hizo.

"Hivi karibuni nilifanya ziara katika baadhi ya mikoa na kuongea na walimu. Walimu waliwasilisha kwangu kero kubwa wanazokabiliana nazo ikiwa ni pamoja na baadhi ya walimu kucheleweshwa kubadilishiwa Muundo wa Utumishi, kutopandishwa madaraja/cheo kwa wakati, kupandishwa daraja la aina moja (kujirudia) tofauti na matarajio yao. Niliiagiza Tume kufuatilia kwenye Tange za walimu ili kuwabaini walimu hao."

"Nawapongeza sana kwa kufanyia kazi maelekezo yangu kwa wakati na kuwezesha taarifa za uchambuzi wa madai hayo ya walimu yanawasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika na linaendelea kufanyiwa kazi," amesema Waziri Kairuki.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu, Waziri Kairuki amemtaka Mkandarasi, SUMA JKT kuhakikisha ujenzi wa Jengo hilo unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaohitajika ili kuisaidia TSC kupata eneo la ofisi kwa kuwa kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya upungufu mkubwa wa vyumba vya ofisi huku akiielekeza TSC kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhakikisha maendeleo ya ujenzi huo yanaendana na mpango kazi uliopo kwenye mkataba wa ujenzi huo.

"Ili kufanikisha ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi hizi kwa wakati, hakikisheni mnafanya ufuatiliaji na tathimini ya ujenzi wa Mkandarasi huyu kila baada ya mwezi na kunijulisha kila hatua iliyofikiwa na endapo kuna changamoto zinazojitokeza ili tuchukue hatua za kutatua bila kuchelewa," alielekeza Waziri huyo.



*Baadhi ya washiriki katika hafla ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS). Hafla hiyo ilifanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

Akitoa neno la kumkaribisha Waziri Kairuki, Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC ambaye pia ni Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama amesema katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita watumishi wa umma wamekuwa wakipandishwa vyeo kwa mfululizo ambapo Walimu 160,888 walipandishwa vyeo kwa mkupuo na walimu 20,032 waliojiendeleza wamebadilishiwa cheo kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo 2020/21 na 2021/22.

Aliongeza kuwa walimu wameendelea kunufaika na juhudi za Serikali kutokana na kulipwa malimbikizo ya madai mbalimbali ya mishahara na yasiyo ya mishahara, kuajiri walimu 14,949 (2020/21) na 9,800 (2021/22), kuweka punguzo la kodi kutoka asilimia 9 hadi 8 na kuondoa tozo ya thamani ya elimu ya juu pamoja na kuongeza umri wa wategemezi wa Bima kutoka miaka 18 hadi 21.

Mwl. Nkwama alisema kuwa pamoja na ufinyu wa Bajeti, katika kipindi cha miaka sita (6) tangu ilipoanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 hadi kufikia mwezi Julai, 2022, Tume hiyo imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali.

"Tume iliratibu na kushughulikia masuala ya kiutumishi ya Walimu ambapo Walimu 43,322 waliajiriwa na kusajiliwa sawa na asilimia 100; Walimu 33,522 (77.4%) walithibitishwa kazini kati ya

# WAZIRI KAIRUKI ASISITIZA WALIMU KUTHAMINIWA NA KUPATIWA MASLAHI YAO KWA WAKATI

43,322 walioajiriwa; Walimu 250,905 walipandishwa cheo; Walimu 22,456 walibadilishwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu; Walimu 30,773 waliandikiwa vibali vya kustaafu kazi; Mafao ya Walimu 2,282 yanayohusu Pensheni, Mirathi na Mikataba yalishughulikiwa na Tume na kulipwa na Hazina."

"Tume ilitoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu 11,396 (98.8%) kati ya 11,529 yaliyoanzishwa. Katika makosa yaliyotendwa, kosa la utoro limeongoza kwa kuwa na walimu 7,579 (66.5%), makosa mengine ambayo ni pamoja na uzembe 56, ulevi 89, mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi 328, kughushi 1,438 na mengineyo yalikuwa na 33.5%. Aidha, hadi sasa Tume imefanikiwa kutolea uamuzi rufaa za Walimu 1038 (95.7%) kati ya 1,074 zilizopokelewa. Rufaa 36 zilizobaki zipo kwenye hatua ya maandalizi ili ziweze kuhitimishwa katika Mkutano wa Tume utakaofanyika mwishoni mwa mwezi Machi, 2023," alisema Mwl. Nkwama.

Pamoja na kufungua Mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi, Waziri Kairuki alizindua mfumo wa Kielektoniki wa Tume hiyo (TSCMIS) ambao unalenga kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake katika kuwahudumia walimu ambapo baada ya uzinduzi huo, mfumo utaanza kutumika katika kushughulikia masuala ikiwemo Ajira na Usajili wa Walimu, Nidhamu, Ukokotoaji wa Mafao na Usajili wa wageni.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Jasmine Kairuki akikabidhi zawadi kwa watumishi wa staafu wa TSC wakati wa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Agellah Jasmine Kairuki (katikati kwa waliokaa), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) katika picha ya pamoja na Menejimenti ya TSC wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Agellah Jasmine Kairuki (katikati kwa waliokaa), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) katika picha ya pamoja na viongozi wa TUGHE wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Agellah Jasmine Kairuki (katikati kwa waliokaa), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# WATUMISHI WA TSC PAMOJA NA WASTAAFU

Picha mbalimbali za watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na watumishi wastaafu wa Tume hiyo wakati wa hafla ya kuwaaga wastaafu iliyofanyika Machi 16, 2023 katika Ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.











# SERIKALI INAFANYA JITIHADA KUBWA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU: NAIBU WAZIRI NDEJEMBI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi amesema Serikali inafanya jitihada kubwa kuleta mageuzi katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kuondoa kero na malalamiko mbalimbali yanayowakabili walimu na kuboresha mazingira ya kufundishia ili walimu watekeleze majukumu yao katika mazingira ya amani na utulivu.

Naibu Waziri ametoa kauli hiyo Machi 9, 2023 alipokutana na Menejimenti ya TSC ikiwa ni ziara yake ya kwanza katika Tume hiyo tangu alipoteuliwa kushika nafasi ya Naibu Waziri OR – TAMISEMi hivi karibuni ambapo amesema dhamira ya serikali ni kuona walimu wote wanatatuliwa kero zao ili watekeleze majukumu yao kwa amani na utulivu.

Amesema kutokana na juhudi hizo za kuboresha mazingira ya walimu, ni muhimu kwa TSC kuendelea kuhakikisha walimu wanapata huduma bora ili waongeze ari katika kuhudumia wanafunzi kwa kuwa walimu wasipokuwa na moyo wa kufundisha Taifa litarudi nyuma kimaendeleo.

“Sote ni mashuhuda kuwa Serikali inafanya kazi kubwa katika kuhakikisha walimu wanatekeleza wajibu wao wakiwa katika mazingira mazuri. Ukiangalia katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia zile kero kubwa za walimu ikiwemo kutopandishwa madaraja amezimaliza. Hivyo, TSC kama chombo kinachosimamia utumishi wa walimu ni lazima muendelee kuongeza juhudi katika kutatua changomoto zilizobaki,” amesema Mhe. Ndejembi.

Pamoja na hayo, Kiongozi huyo amesema Rais Samia anatambua umuhimu na kazi kubwa inayofanywa na Tume hiyo kwa walimu, ndiyo maana ameruhusu miradi ya ujenzi wa jengo la Ofisi, ujenzi wa Mfumo wa kielektoniki wa kurahisisha utoaji huduma kwa walimu na miradi mingine ya wadau maendeleo kuisaidia kufanyika ili kuifanya TSC iimarike na kushughulikia walimu kwa ufanisi zaidi.

Akihitimisha hotuba yake fupi, Mhe. Ndejembi amesema kuwa atafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na TSC na kueleza kuwa kwake milango iko wazi muda wote kwa kiongozi anayehitaji kuonana nae kwa lengo la kushauriana masuala mbalimbali kwa ajili ya maslahi ya walimu.

\Akimkaribisha Naibu Waziri huyo ili azungumze na Menejimenti ya Tume hiyo, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama ameeleza kuwa Tume hiyo inatekeleza miradi miwili kwa fedha za ndani na mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa fedha za nje.

Akifafanua miradi hiyo Nkwama alisema, kupitia fedha za ndani TSC inatekeleza ujenzi wa jengo lake la Utawala la Ofisi ya Makao Makuu ambapo shughuli



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi (kushoto) akipokea ua kutoka kwa mtumishi wa TSC, Enid Geofrey wakati alipofanya ziara ya kujitambulisha katika ofisi za TSC Machi 9, 2023. Pichani, katikati ni Ktibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi (kushoto) akipokea nyaraka mbalimbali za TSC kutoka wa Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama wakati alipofanya ziara ya kujitambulisha katika ofisi za TSC Machi 9, 2023.*

# SERIKALI INAFANYA JITIHADA KUBWA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU: NAIBU WAZIRI NDEJEMBI



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akizungumza jambo wakati wa kikao cha Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI na Wakurugezi wa TSC kilichofanyika wakati Naibu Waziri huyo alipofanya ziara ya kujitambulisha katika ofisi za TSC Machi 9, 2023.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Degratius Ndejembi akizungumza katika kikao na Menejimenti ya TSC wakati alipofanya ziara ya kujitambulisha katika ofisi za TSC Machi 9, 2023.*

za ujenzi zinaendelea kupitia kwa mkandarasi SUMA JKT.

Amemweleza Naibu waziri huyo kuwa mradi mwingine ni Ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama Teachers' Service Commission Management Information System (TSC-MIS) ambao umekamilika katika awamu ya kwanza huku ukijumuisha moduli sita ambazo zinajumuisha Usimamizi wa Mashauri, Usimamizi wa Rufaa, Msaada kwa Wateja na Malalamiko, Uratibu wa Wageni, Ajira na Usajili pamoja na Usimamizi wa Mafao na Mirathi.

Akizungumzia mradi wa BOOST, Mwl. Nkwama amesema katika kipindi cha nusu mwaka (Julai – Desemba, 2022) TSC ilipokea fedha za mradi huo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kiasi cha shilingi 633,002,856 kati ya shilingi 3,416,853,760 zilizoidhinishwa kwa ajili ya TSC kwa mwaka wa kwanza (2022/2023) wa utekelezaji wa mradi.

"Kwa mwaka huu mradi wa BOOST unawezesha kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo; Kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu, kununua magari 15, laptops 159 na vifaa vingine vya TEHAMA pamoja na kufanya mapitio na kuhuisha Sheria zinazosimamia Utumishi wa Mwalimu kwa ajili ya kuandaa Sera ya kitaifa ya Mwalimu," amesema.

Nkwama amehitimisha kwa kumshukuru Rais Samia kwa jitihada zake katika kuwahudumia walimu pamoja Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ushirikiano wanauonesha kwa TSC katika utekelezaji wa majukumu ya utumishi wa walimu.





*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi akisalimiana wa watumishi wa TSC wakati alipofanya ziara ya kujitambulisha katika ofisi za TSC Machi 9, 2023.*

# DKT. MSONDE AONGOZA KIKAO CHA KUPITIA MAPENDEKEZO YA MAPITIO YA SHERIA MBALIMBALI ZINAZOHUSU WALIMU



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde (kulia) akiongoza kikao kilichowahusisha wajumbe wa Menejimenti ya TSC kwa lengo la kupitia mapendekezo ya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu walimu. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma. Pembeni yake ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria wa TSC, Wakili Richard Odongo akiwasilisha muhtasari wa mapendekezo ya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu walimu katika kikao kilichoongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde kilichofanyika katika Ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dkt. Charles Msonde (kushoto) akiongoza kikao kilichohusisha Menejimenti ya TSC kwa lengo la kupitia mapendekezo ya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu walimu. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika Ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Kikao kilichoawakunanisha wajumbe wa Menejimenti ya TSC kwa lengo la kupitia mapendekezo ya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu walimu kikiwa kinaendelea.*



*Kikao kilichoawakunanisha wajumbe wa Menejimenti ya TSC kwa lengo la kupitia mapendekezo ya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu walimu kikiwa kinaendelea.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akizungumza jambo na Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Bibi Fatuma Iddi Muya.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jamsine Kairuki (wa pili kutoka kushoto) akizungumza jambo na Mwanyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto) na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia) pamoja na Katibu wa Baraza hilo, Laurence Chankan mara baada ya ufunguzi wa Baraza hilo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jamsine Kairuki (Katikati) akimsikiliza Mwanyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama mara baada ya ufunguzi wa Baraza hilo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma. Wa kwanza upande wa kulia ni Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Willy Komba.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa TSC, Wakili Richard Odongo akitoa mada kuhusu Maadili ya Utumishi wa Umma wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitego cha Mipango Ufuatiliaji na Tathmini wa TSC, Evodia Pangani akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitego cha TEHAMA wa TSC, Kainda Ndasa akitoa maelezo mafupi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jamsine Kairuki (hayupo pichani) wakati wa hafla ya uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jamsine Kairuki (Katikati) akiimba wimbo wa Mshikamano wakati wa Ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*





*Washiriki wa Mkutano wa Baraza la wafanyakazi la TSC wakiimba wimbo wa Mshikamano Daima wakati wa Ufungungi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# WAZIRI KAIRUKI AONGOZA KIKAO KUPITIA RANDAMA YA TSC



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Angellah Kairuki (kushoto) akiongoza kikao cha kupitia Mpango na Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Ofisi za OR – TAMISEMI Dodoma na kulihusisha Menejimenti ya Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi hiyo.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiwasilisha taarifa ya Mpango na Bajeti ya TSC ya mwaka wa fedha 2023/2024 katika kikao kilichofanyika hivi karibuni kikiongozwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Angellah Kairuki.*





*Kikao cha kupitia Mpango na Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ya mwaka wa fedha 2023/2024 kikiwa kinaendelea.*



*Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ngorongoro kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Msingi wilayani hapo imetembelea shule ya msingi Arashi, na kuongea na walimu juu ya ufafanuzi wa kanuni za maadili ya utumishi wa walimu. Pichani ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Ngorongoro, Rachel Mziray (wa pili kutoka kulia mstari wa mbele) pamoja na walimu wa shule hiyo.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Ngorongoro, Rachel Mziray (wa tatu kutoka kulia mstari wa mbele) pamoja na walimu wa shule ya Msingi Ormanie wakati wa ziara yake katika shule hiyo iliyofanyika hivi karibuni.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Ngorongoro, Rachel Mziray akiongea na wanafunzi wa darasa la tatu wa shule ya Msingi Ormanie wakati alipofanya ziara shuleni hapo hivi karibuni.*

# MKANDARASI WA UJENZI WA JENGO LA TSC, SUMA JKT ATAKIWA KUONGEZA NGUVUKAZI KUKAMILISHA MRADI KWA WAKATI



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi (katikati) akiwasili katika eneo la Ndejengwa jijini Dodoma ambapo ndipo unapotekelezwa mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu. Katika ziara hiyo iliyofanyika Machi 9, 2023 Naibu Waziri huyo aliambatana na Mejejimenti ya TSC.*

**Na Mwandishi wetu – Dodoma.**

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR–TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi amemtaka Mkandarasi, SUMA JKT anayejenga jengo la Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuongeza nguvukazi ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Mhe. Ndejembi ameyasema hayo Machi 9, 2023 alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu katika eneo la Ndejengwa jijini Dodoma ambapo alibaini kuwa mradi huo upo nyuma ikilinganishwa na mpango kazi wa utekelezi wa kazi hiyo.

"Hapa ni lazima muone namna ya kufanya ili utekelezaji wa mradi huu uendane na mpango kazi mliokubaliana kwenye mkataba. Kwa mujibu wa mpango kazi ilitakiwa wakati huu mmefikia asilimia 16 ya utekelezaji wa mradi, lakini hadi sasa bado mpo nyuma. Ongezeni nguvukazi ili kuharakisha ujenzi kwa kuwa tunataka kila hatua iendane na mpango kazi wetu na hatimae mradi ukamilike kwa wakati uliopangwa bila kuongeza muda," amesema Naibu Waziri huyo.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa jengo hilo ni muhimu sana kwa kuwa kwa sasa TSC inafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na upungufu wa vyumba vya ofisi kwa ajili ya watumishi na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali za walimu, hivyo ujenzi huo unatakiwa ukamilike kwa wakati ili kuondokana na adha hiyo.

"Mazingira wanayofanyia kazi TSC kwa sasa hayaendani na uzito wa majukumu waliyonayo, wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya ofisi za watumishi na vyumba vya kutunzia nyaraka mbalimbali. Hivyo, tunawategemea sana



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi akitoa maelekezo kwa Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu, SUMA JKT wakati wa ziara yake katika eneo la mradi, Ndejengwa jijini Dodoma Machi 9, 2023.*

# MKANDARASI WA UJENZI WA JENGO LA TSC, SUMA JKT ATAKIWA KUONGEZA NGUVUKAZI KUKAMILISHA MRADI KWA WAKATI



*Msimamizi wa Mradi kutoka SUMA JKT, Maj. Samwel Jambo (mwenye sare za jeshi) akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Nchi OR – TAMISEMI, Mhe. Deogratius Ndejembi kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu katika eneo la Ndejengwa jijini Dodoma wakati Naibu Waziri huyo alipofanya ziara katika eneo hilo Machi 9, 2023.*

mkamilishe mradi huu kwa wakati ili tuwaondolee adha ya kufanya kazi katika mazingira magumu," amesema.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri huyo alisema kwamba atafanya ziara katika mradi huo kila baada ya miezi mitatu ili kuhakikisha ujenzi huo unafanyika kwa kasi na viwango vinavyotakiwa kwa mujibu wa mkataba.

Akizungumza kuhusu sababu ya mradi huo kuwa nyuma ya mpango kazi, Msimamizi wa Mradi kutoka SUMA JKT, Maj. Samwel Jambo amesema kuwa wakati wa kuchimba mashimo ya nguzo za jengo walikuta mwamba mgumu ambao ulilazimu kutafuta vifaa vya ziada kwa ajili ya kuutoboa, hivyo kupunguza kasi ya ujenzi huo.

Hata hivyo, msimamizi huyo amesema kuwa wamepokea maelekezo ya Naibu Waziri na watayafanyia kazi kwa haraka ili kuhakikisha ujenzi huo unaendana na mpango kazi wa mkataba na hivyo kufanya mradi ukamilike kwa wakati.

Naye Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama amesema ujenzi ukikamilika utasaidia Tume kutoa huduma kwa walimu kwa ufanisi zaidi huku akieleza kuwa ana imani kuwa mkandarasi huyo atakamilisha kazi kwa wakati.

"Mhe. Naibu Waziri sisi TSC tuna imaini kuwa walichokisema wenzetu SUMA JKT watakwenda kukitekeleza. Kwa kweli tangu tumeanza mradi huu tunakwenda nao vizuri, tunaamini kwamba watakamilisha kwa wakati ili tuweze kuhudumia walimu wetu kwa ufanisi zaidi," amesema Mwl. Nkwama.

Mradi huo unaogharimu kiasi cha shilingi 6,499,982,353.03 ambao unatekelezwa kwa kipindi cha miezi 18 umeanza Desemba 6, 2022 na utakamilika ifikapo Juni 2, 2024. TSC tayari imelipa kiasi cha shilingi 500,000,000 ikiwa ni malipo ya wali ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.





*Mwonekano wa hatua iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu unaofanyika katika eneo la Ndejengwa jijini Dodoma.*

# WALIMU WILAYANI KALAMBO WAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA BIDII



*atibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na walimu wa Wilaya ya Kalambo Machi 23, 2023 wilayani hapo kwa lengo la kuwaelimishi juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu.*

**Na Mwandishi wetu – Kalambo.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amewapongeza walimu wa Wilaya ya Kalambo kwa jitihada wanazofanya katika kutoa huduma bora kwa wanafunzi na kukuza maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Ameotoa pongezi hizo Machi 23, 2023 katika kikao chake na baadhi ya walimu wa Wilaya ya Kalambo ambapo Katibu huyo yupo Wilayani hapo kwa ajili ya kushiriki mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) yanayofanyika katika chuo cha Ualimu, Sumbawanga kwa siku tatu, Machi 21 – 23, 2023 huku yakihusisha watumishi wa TSC kutoka wilaya za Mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma.

Alieleza kuwa Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na walimu na hivyo imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu zaidi lengo likiwa wanafunzi wanapata elimu inayotarajiwa.

"Tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa kuendelea kufundisha wanafunzi wetu kwa bidii, weledi na uzalendo. Utendaji wenu mzuri wa kazi ni moja ya njia kuhakikisha Taifa letu linapiga hatua zaidi kimaendeleo hususan katika sekta ya elimu. Tunawashukuru sana na tunawaomba muendelee na moyo huo wa kufanya kazi kwa moyo wa kujituma ili tuendelee kuinua taaluma katika Wilaya ya Kalambo na Taifa kwa ujumla," alisema Nkwama.

Nkwama aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya juhudi mbalimbali kuboresha utendaji



*Baadhi ya Walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo wakimsikiliza Katibu wa TSC katika kikao kilichofanyika Machi 23, 2023 wilayani Kalambo.*

# WALIMU WILAYANI KALAMBO WAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA BIDII



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto) akiwa katika mazungumzo na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Bw. Sunday Wambura. Upande wa kushoto ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Bi Fatuma Muya.*

kazi wa walimu ikiwa ni pamoja na kuanzisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki kurahisisha utoaji wa huduma, kulipa madeni ya walimu, kupandisha madaraja, kubadilisha cheo walioiendeleza kielimu, kugawa vishkwambi kwa walimu, ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara na nyumba za walimu, punguzo la kodi kwenye mishahara ya watumishi wa umma pamoja utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa walimu.

"Tunapaswa tumuunge mkono Rais wetu kwa kuwa amefanya na anaendelea kufanya mambo mengi mazuri kwa ajili yetu sisi walimu. Fedha nyingi ambazo zimeelekezwa katika sekta ya elimu zinapaswa zitoe matokeo chanya kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla, hivyo walimu ndio tuna wajibu kuhakikisha nguvu zote zilizoelekezwa kwenye sekta hii zinaleta mafanikio yanayokusudiwa," alisema.

Akizungumzia kuhusu mfumo wa TSCMIS Nkwama alisema utarahisisha utoaji wa huduma kwani kupitia simu ya mkononi mwalimu ataweza kuwasilisha hoja zake na zikafanyiwa kazi kwa wakati na kupata mrejesho bila kutoka kwenye kituo chake cha kazi, hivyo itasaidia walimu kutulia shuleni na kufundisha badala ya kutumia muda wa kufundisha kwenye ofisi nyingine kutafuta huduma.

Pamoja na Mafunzo na Kikao hicho, Katibu wa Tume na Ujumbe wake walitembelea Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya hiyo na kuzungumza na watendaji wa Ofisi hiyo kuhusu Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu na namna ya Kufanya kazi pamoja na ofisi hiyo katika kuwahudumia walimu.

Vilevile kiongozi huyo alitembelea Ofisi ya TSC Wilaya ya Kalambo baada ya kutembelea Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ambapo alimshukuru Mkurugenzi huyo kwa kuipatia Tume vyumba vitatu vya Ofisi katika Jengo jipya la Utawala kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

Baada ya kazi, Katibu na ujumbe wake walitembelea vivutio vya Utalii wa ndani ambavyo ni Maporomoko ya maji ya Kalambo, Fukwe na bandari ya ziwa Tanganyika eneo la Kasanga - Kalambo, Rukwa.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa ofisi ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. Wa kwanza upande wa kulia ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Bi Fatuma Muya.*








*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifanya utalii wa ndani kwa kutembelea maporomoko ya maji ya Kalambo.*

# WAZIRI KAIRUKI ATOA VYETI NA TUZO KWA WALIOHUSIKA NA UJENZI WA MFUMO WA TSCMIS








*Picha mbalimbali za Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki akikabidhi vyeti na tuzo kwa watumishi mbalimbali waliohusika katika kutengeneza Mfumo wa Kielektoniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS). Hayo yalifanyaka wakati wa uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# WAZIRI KAIRUKI ATOA VYETI NA TUZO KWA WALIOHUSIKA NA UJENZI WA MFUMO WA TSCMIS








*Picha mbalimbali za Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki akikabidhi vyeti na tuzo kwa watumishi mbalimbali waliohusika katika kutengeneza Mfumo wa Kielektoniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS). Hayo yalifanyaka wakati wa uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# WALIMU UKEREWE WATAKIWA KULINDA HADHI YA UALIMU KABLA NA BAADA YA KUHITIMISHA UTUMISHI WAO



*Picha ya pamoja ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen M. Kushoka na walimu walioshiriki kikao kazi cha kuelimisha walimu juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.*

**Na Mwandishi wetu – Ukerewe.**

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen M. Kushoka ametakata walimu wilayani hapo kulinda hadhi na heshima ya utumishi wa walimu kabla na baada ya kustaafu kazi hiyo.

Kushona ameyasema hayo tarehe 15.03.2023 wakati wa kikao kazi kilichowahusisha walimu 60 kutoka katika shule sita za msingi na moja ya sekondari kilicholenga kutoa elimu juu ya kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

Alisema mwalimu ni mfano wa kuigwa ambapo jamii inategemea kujifunza mambo mengi kutoka kwake hivyo, hata kama mwalimu amestaafu hanabudi kuhakikisha anaendelea kujiheshimu ili kuendelea kuwa chachu ya maadili katika jamii.

"Mwalimu anayelinda taaluma yake ni sawa na Mwalimu anayelinda hadhi na heshima yake mwenyewe na Mwalimu wa namna hii ataheshimiwa na Wanafunzi wake lakini pia jamii nzima inayomzunguka itamuheshimu wakiwemo," alisema.

Aidha, Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliwataka Walimu kujiepusha na mikopo umiza badala yake wakope kwenye taasisi za kibenki za zinazotambuliwa na Serikali ili kulinda hadhi na taaluma yao.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen M. Kushoka akiongea na wanafunzi wakati wa kikao kazi cha cha kuelimisha walimu juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen M. Kushoka akiongea na wanafunzi wakati wa kikao kazi cha cha kuelimisha walimu juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.*

# WAJUMBE BARAZA LA WAFANYAKAZI WATEMBELEA UJEZI WA OFISI ZA TSC NJEDENGWA, DODOMA













*Picha mbalimbali za Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) walipotembelea mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaoendelea kutekelezwa katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma. Ziara hiyo ilifanyika Machi 16, 2023 wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi.*

# MRADI WA BOOST WAIWEZESHA TSC KUANZA KUPITIA SHERIA ZOTE ZINAZOMGUSA MWALIMU



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao kazi kikao kazi cha kupitia andiko la rasimu ya mapendekezo ya kuhuisha sheria na kanuni zote zinazohusu mzunguko wa mwalimu kilichofanyika Machi 1 – 3, 2023 mjini Morogoro.*



*Kiongozi wa timu ya wataalamu walioandaa andiko la rasimu ya mapendekezo ya kuhuisha sheria na kanuni zote zinazohusu mzunguko wa mwalimu ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa TSC, Richard Odongo akitoa maneno ya utangulizi kuhusu kazi hiyo ya kupitia sheria na kanuni zinazohusu walimu.*

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza mchakato wa kupitia sheria na kanuni zote zinazomsimamia mwalimu ili kufanya maboresho katika kumhudumia mwalimu kwa ufanisi zaidi.

Akizungumza katika kikao kazi cha kupitia rasimu ya mapendekezo yaliyoandaliwa na timu ya wataalamu wa sheria, elimu na usimamizi wa rasilimali watu baada ya kupitia sheria hizo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alisema kazi hiyo inafanyika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa BOOST ambao unafadhili shughuli mbalimbali za elimu nchini.

Kikao kazi hicho kinaikutanisha Menejimeti ya TSC na timu ya wataalamu hao na kilifanyika kwa siku tatu kuanzia Machi 1 hadi 3, 2023 katika ukumbi wa Mahakama mjini Morogoro.

Mwl. Nkwama amefafanua kuwa mradi wa BOOST una afua nane (8) na moja ya afua hizo ni Shule Salama ambapo TSC ni miongoni mwa wanufaika kwa kuwezeshwa kuandaa miongozo na nyaraka mbalimbali za kusimamia utumishi wa walimu, kutoa mafunzo kuhusu masuala mbalimbali ya walimu, kununua vitendea kazi ikiwemo magari na kompyuta.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao kazi kikao kazi cha kupitia andiko la rasimu ya mapendekezo ya kuhuisha sheria na kanuni zote zinazohusu mzunguko wa mwalimu kinachofanyika Machi 1 – 3, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria TSC,Wakili Richard Odongo na kulia ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Fatuma Muya.*



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kupitia rasimu ya mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazumhusu mwalimu wakiendelea na kikao.*

# MRADI WA BOOST WAIWEZESHA TSC KUANZA KUPITIA SHERIA ZOTE ZINAZOMGUSA MWALIMU

Ameongeza kuwa shughuli mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa ufadhili wa mradi huo ni matokeo ya jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kutafuta wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuleta mageuzi katika sekta ya elimu kwa lengo la kumfanya mwalimu aweze kutoa huduma bora ya kuwalea wanafunzi katika nyanja zote kama ilivyokusudiwa.

"Tupo hapa kwa ajili ya kufanya mapitio ya mapendekezo yanayotokana na kazi inayoendelea kufanyika ya kupitia sheria mbalimbali zinazomgusa mwalimu na utumishi wake kwa ujumla. Haya yote tunayafanya kwa lengo la kutafuta njia nzuri itakayomfanya mwalimu aifurahie kazi yake na atekeleze majukumu yake kwa amani, utulivu na ufanisi zaidi," amesema.

Katibu huyo aliweka wazi kuwa maboresho mbalimbali yanayofanyika kwenye sekta ya elimu yanalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi inayotoa elimu bora kitaifa na kimataifa, na mtoto anapomaliza elimu yake aweze kukabiliana na changamoto binafsi, mazingira yanayomzunguka, na kuweza kushindana katika soko la ajira kimataifa.

Naye kiongozi wa wataalamu walioandaa andiko la rasimu ya mapendekezo hayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa TSC, Wakili Richard Odongo alisema kuwa timu hiyo ilipitia Sheria na Kanuni zote zinazomhusu mwalimu na kutoa mapendekezo yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuongeza tija katika kumhudumia mwalimu.

Timu hiyo ilihusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu.






*Washiriki wa Kikao Kazi cha kupitia rasimu ya mapitio ya Sheria na Kanuni zote zinazumhusu mwalimu wakiendelea na kikao.*

# KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA, ELIMU NA UTAFITI



*Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Utawala Elimu na Utafiti ya TSC, Kamishna Assela Luena (katikati) akiongoza kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma. Upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na kushoto ni mjukbe wa kamati hiyo, Kamishna Bahati Mgongolwa.*





*Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Utawala Elimu na Utafiti ya TSC, Kamishna Assela Luena akiongoza kikao cha kamati hiyo kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma.*



*Kikao cha Kamati ya Fedha Utawala Elimu na Utafiti ya TSC kikiwa kinaendelea.*

# TSC YAWAAGA WASTAAFU











*Picha mbalimbali za Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki akikabidhi zawadi kwa watumishi wa staafu wa TSC wakati wa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# TSC YAWAAGA WASTAAFU











*Picha mbalimbali za Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki akikabidhi zawadi kwa watumishi wa staafu wa TSC wakati wa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC na uzinduzi wa Mfumo wa Kielektoniki wa TSC (TSCMIS) Machi 16, 2023 jijini Dodoma.*

# WAZIRI JAFO AWATAKA WADAU WA ELIMU KISARAWE KUONGEZA UWEKEZAJI KWENYE ELIMU



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mazingira ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kisarawe Mhe. Selemani Jafo.*

**Na Mwandishi wetu – Kisarawe.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira, Mhe. Selemani Saidi Jafo amewataka wadau wa Elimu katika Wilaya ya Kisarawe kutumia rasilimali za kutosha ili kuwekeza katika elimu kwa nia ya kupata wataalamu watakaoweza kusimamia rasilimali na fursa zinazopatikana hapa nchini.

Waziri Jafo ambaye pia ni Mbunge wa jimbo la Kisarawe aliyasema hayo Machi 7, 2023 katika ukumbi wa shule ya sekondari Minaki wilayani hapa, alipokuwa akizungumza na wadau wa Elimu wa Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe ambapo aliwapongeza wadau wa elimu wakiwemo TSC, Mkurugenzi, Wakuu wa Idara za Elimu, walimu na wadau wengine kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kufundisha kiasi kwamba wameweza kuongeza ufaulu kutoka asilimia 85 hadi 87 kwa darasa la saba kwa matokeo ya mwaka 2022.

Alisema kuwa kwa upande wa sekondari ufaulu kwa kidato cha nne haukushuka wala kupanda huku matokeo ya kidato sita ufaulu ukiwa ni asilimia 98.8 kwa mwaka 2022.

"Matokeo haya yana nafuu kulinganisha na hali ilivyokuwa huko nyuma. Hivyo ninawasihi muendelee kufanya kazi kwa bidii, weledi na uzalendo ili Wilaya yetu iendelee kufanya vizuri katika sekta ya elimu na sekta nyingine," alisema Waziri Jafo.

Kwa lengo la kupata matokeo chanya zaidi, waziri Jafo alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mahusiano kati ya walimu, wazazi na wanafunzi ambapo alisema kukiwa na upendo na umoja matokeo yatakuwa mazuri zaidi. Alitolea mfano wa baadhi ya shule zenye hosteli kwa ajili ya wanafunzi kukaa hapo lakini kwa sababu ya kukosekana umoja huo, baadhi ya wanafunzi wanapanga vyumba mtaani badala ya kuishi katika mabweni yaliyojengwa kwa ajili yao.

Awali, Mkuu wa idara ya elimu ya awali na msingi Bi. Hadija Mwinuka, aliwasilisha taarifa ya tathimini ya hali ya elimu ya wilaya hiyo kwa mwaka 2023 ambapo alisema uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali ulifikia asilimia 139 huku darasa la kwanza ilifikia asilimia 113 huku upande wa sekondari walioripoti shuleni kwa Kidato cha Kwanza walifikia asilimia 91.



*Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mhe. Fatuma Nyangasa akizungumza katika kikao cha wadau wa Elimu wa Wilaya ya Kisarawe kilichofanyika hivi karibuni wilayani hapo.*



*Mshiriki wa kikao cha wadau wa Elimu wa Wilaya ya Kisarawe akitoa maoni yake wakati wa kikao hicho kilichofanyika wilayani hapo hivi karibuni.*

# WAZIRI KAIRUKI AIPONGEZA TSC KWA UWAJIBIKAJI, ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA TUME



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (kushoto) akipokea nyaraka mbalimbali zinazoongoza utekelezaji wa majukumu ya TSC kutoka kwa mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba Machi 31, 2023 jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya walimu na kuitaka kuendeleza ari hiyo ili kuendelea kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji nchini.

Waziri Kairuki ametoa pongezi hizo tarehe 31 Machi 2023 alipotembelea Mkutano wa Tume uliokuwa unafanyika katika ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) jijini Dodoma kwa lengo la kujionea namna Tume hiyo inavyoendesha vikao vyake katika kuamua masuala mbalimbali ya walimu ambapo ziara hiyo iliambatana na ukaguzi wa ujenzi wa Jengo la Utawala la Tume hiyo unaofanyika katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (kulia) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama wakionesha nyaraka mbalimbali zinazoongoza utekelezaji wa majukumu ya TSC wakati Waziri Kairuki alipotembelea Mkutano cha Tume Machi 31, 2023 katika Ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*

"Ninawapongeza Makamishna pamoja na watendaji wote wa Tume hii kwa namna mnavyotekeleza majukumu ya kuwahudumia walimu. Sote ni mashahidi kuwa kazi mnayoifanya inaonekana na tunaona walimu wetu wamekuwa na utulivu na wanaendelea kufanya kazi kwa kujituma. Ninawasihi tuendelee kufanya kazi kwa bidii na kutatua changamoto za walimu ili waendelee kuwa na ari ya kufundisha watoto wetu," amesema Kairuki

Pamoja na pongezi hizo, Waziri Kairuki ameitaka TSC kuendelea kuongeza ubunifu katika utendaji kazi kwa kujifunza kwa Taasisi za ndani na nje ya nchi zinazotekeleza majukumu yanayoendana na ya TSC pamoja na kuendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika kutoa huduma kwa walimu.

"Kwa jinsi nilivyowasikiliza ninaona kuna vitu mnaweza kuviboresha ili kuongeza ubora wa kazi yenu. Mnaweza kwenda kujifunza namna mahakama wanavyoendesha masuala ya kesi ili nanyi muone namna mnavyoweza kuboresha uendeshaji wa mashauri ya nidhamu. Pia, mnaweza kuangalia vyombo vinavyosimamia walimu katika nchi zingine muone ni kipi mnaweza kujifunza. Ni muhimu pia muone namna ya kuwajengea uwezo watumishi hususan namna ya kuchukua dondoo na kuandaa hansadi kwa ajili ya kumbukumbu na rejea," amesema.

# WAZIRI KAIRUKI AIPONGEZA TSC KWA UWAJIBIKAJI, ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA TUME



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (kushoto) akiwa katika mazungumzo na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba Machi 31, 2023 jijini Dodoma.*

Kuhusu changamoto mbalimbali zinazoikabili Tume hiyo ikiwemo ufinyu wa bajeti, upungufu wa watumishi, upungufu na uchakavu wa ofisi za Wilaya, Waziri ameahidi kuzifanyia kazi kwa kuwasiliana na mamlaka zingine zinazohusika ili kupata ufumbuzi wake kwa haraka.

Baada ya kutembelea utekelezaji wa ujenzi wa jengo la Utawala la TSC, Kairuki ameipongeza SUMA JKT kwa utekelezaji wa mradi huo huku akiwataka kuongeza kasi ili kuendana na mpango kazi wa wa utekelezaji wa mradi.

Katika mradi huo ambao umefikia asilimia nane (8) ya utekelezaji wake, kazi mbalimbali zimefanyika ikiwemo ukusanyaji wa vifaa na mahitaji ya kazi, uchimbaji wa mashimo 84 ya msingi na umwagaji wa zege la awali, ufungaji wa chuma za msingi na chuma za nguzo pamoja na umwagaji wa zege la msingi wa nguzo.

Kairuki amesema kuwa jengo hilo ni lazima likamilike katika kipindi kilichopangwa na kusisitiza kuwa ataendelea kufanya ziara za mara kwa mara ili kuona kasi ya utekelezaji wa kazi hiyo.

"Mnafanya kazi nzuri lakini inabidi muongeze kasi zaidi kwa kuwa bado mko nyuma ikilinganishwa na mpango kazi, ninajua mnao uwezo wa kuongeza nguvu kazi ili kasi ya ujenzi iongezeke. Jengo hili ni muhimu sana kwa TSC kwani hawana mazingira mazuri ya kufanyia kazi kitu ambacho kinaathiri utendaji wao wa kazi. Tunatamani jengo hili likamilike ili walimu wetu waweze kuhudumiwa vizuri zaidi," alisema Waziri Kairuki.

Awali, akitoa neno la kumkaribisha Waziri huyo, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu Tume imefanikiwa kutoa uamuzi wa rufaa za Walimu 509 (91.1%) kati ya 559 sawa na asilimia 91.1, kupandisha vyeo Walimu 160,888 na kuwabadilishia vyeo Walimu 20,032 baada ya



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akiwa katika kikao na Makamishna wa TSC Machi 31, 2023 jijini Dodoma.*

# WAZIRI KAIRUKI AIPONGEZA TSC KWA UWAJIBIKAJI, ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA TUME



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akipitia nyaraka wakati Mkutano wa Tume ukiwa unaendelea kujadili rufaa za walimu Machi 31, 2023 jijini Dodoma.*



*Mkutano wa Tume ukiwa unaendelea kujadili rufaa za walimu ambapo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki alihudhuria mkutano Machi 31, 2023 kuona namna rufaa za walimu zinavyoendeshwa. Mkutano huo ulifanyika katika Ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*

kujiendeleza kielimu, kupandisha vyeo watumishi wa Tume 304 na kuwabadilishia cheo/kazi watumishi 24 waliojiendeleza kielimu, kuratibu na kusajili ajira za walimu 24,749 pamoja na kuratibu uthibitisho wa Walimu 14,949 (60.4%) kati ya 24,749 walioajiriwa ambapo walimu 9,800 ambao hawajathibitishwa kazini ni ajira ya Julai, 2022 ambao wanatarajiwa kuthibitishwa kazini Julai, 2023.

Aidha Imesema TSC imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama (Teachers Service Commission Information Management System (TSC-MIS), kusimamamia upatikanaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Tume Makao Makuu, ambapo Tume ilinunua kiwanja hicho kutoka ofisi za Jiji la Dodoma pamoja na kuandaa ufafanuzi wa Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu, jukumu ambalo Tume imelitekeleza kwa mujibu wa Kifungu Na.5(x) cha Sheria ya Tume Sura 448.

Naye Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama amemshukuru Waziri huyo kutokana na ushirikiano wake kwa Tume hiyo kitu ambacho kimewezesha bajeti ya Tume kuendelea kupanda na ameahidi kuwa wataendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na uzalendo ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu iliyokusudiwa.

"Kupitia jitihada zako Mhe. Waziri tumeongezwa bajeti kutoka shilingi 14,773,473,000.00 mwaka wa fedha wa 2020/2021 hadi kufikia shilingi 17,203,948,000 kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 14.1. Pia tunamshukuru Mhe. Rais pamoja na Ofisi yako kwa kutujumuisha kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa inatusaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu wetu," amesema Nkwama.



*Mkutano wa Tume ukiwa unaendelea kujadili rufaa za walimu ambapo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki alihudhuria mkutano huo Machi 31, 2023 kuona namna rufaa za walimu zinavyoendeshwa. Mkutano huo ulifanyika katika Ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Makamishna, Wajumbe wa Menejimenti pamoja na baadhi ya Watumishi wa TSC wakati alipotembelea mkutano wa Tume Machi 31, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (wa tatu kutoka kushoto) akitoa maelekezo kwa Mkandarasi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu, SUMA JKT alipotembelea mradi huo Machi 31, 2023.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (mwenye kofia ya njano) akipokea maelezo juu ya maendeleo ya ujenzi wa Ofisi za TSC kutoka kwa mmoja wa watendaji wa Kampuni ya SUMA JKT ambayo ndiyo mkandarasi mradi huo.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akiendelea kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi ya TSC Makao Makuu Machi 31, 2023.*

# TSC YAENDESHA MAFUNZO YA TSCMIS

**Na Mwandishi wetu – Tanga.**

Tukiendelea kuadhimisha Siku 730 za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan madarakani na baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) Machi 16, 2023 kuzindua Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) na kuanza kutumika rasmi kwa ajili ya kushughulikia mnyororo mzima wa Utumishi wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini waliopo katika Utumishi wa Umma;

Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Machi 21, 2023 iliendesha mafunzo kwa Watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kwenye Mikoa Nane (8) ukiacha mmoja (Dodoma) ambao ulishapata mafunzo hayo chini ya ufadhili wa Programu ya Shule Bora (SB); Pwani, Tanga, Rukwa, Katavi, Kigoma, Mara, Simiyu na Singida inayoendelea sasa.

Pichani ni Washiriki wa mafunzo hayo kutoka Ofisi za TSC Mikoa mbalimbali wakiwa katika mafunzo yanayofanyika katika vituo vitatu, Kituo cha Korogwe kinachohusisha Mikoa ya Tanga na Pwani, kituo kingine cha Sumbawanga kilichojumuisha mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma na kituo cha Bunda kilichojumuisha mikoa ya Mara, Simiyu na Singida. Kwa vituo vyote vitatu jumla ya Washiriki 86 walihudhuria mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku nne kuanzia Machi 21 hadi 24, 2023.

Mfumo huu mpya wa TEHAMA ujulikanao kama 'Teachers Service Commission Management Information System - TSCMIS' umejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha kazi ya kushughulikia mnyororo mzima wa Utumishi wa Walimu ikiwemo: Ajira za Walimu, Kuthibitisha Walimu Kazini, Kupandisha Walimu Vyeo, Kubadilisha Walimu Vyeo, Mirathi na Pensheni, Malalamiko ya Walimu, Usajili wa Wageni pamoja na kushughulikia Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za ya Walimu.





# TSC YAENDESHA MAFUNZO YA TSCMIS



































*Picha mbalimbali za mikutano ya Tume ya Utumishi wa Walimu TSC Wilaya ya Bukombe iliyolenga kuwajengea uwezo walimu wa Kata ya Uyovu na Busonzo juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ambapo zaili ya Walimu 300 walifikiwa. Ziara hizo zilifanyika Machi, 2023 ambao Maafisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe walishuriki ziara hizo.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki na wawezeshaji wa mafunzo Mfumo wa Kielektoniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) wanawake. Mafunzo hayo yamefanyika hivi karibuni wiayani Sumbawanga. Pichani, wa kwanza upande wa kulia ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Fatuma Muya.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo ya TSCMIS kutoka Wilaya za Mkoa wa Rukwa.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa TSCMIS kutoka Wilaya za Mkoa wa Sumbawanga.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Shule Bora Mkoa wa Rukwa Bw. Mfwimi Malinzanga (katikati) na Bi. Chabe Mbulinyingi. Mradi wa Shule Bora ndio unaogharamia uendeshaji wa mafunzo ya TSCMIS.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa TSCMIS kutoka Wilaya za Mkoa wa Katavi.*

# NKWAMA AWATAKA WATUMISHI SUMBAWANGA KUONGEZA JUHUDI KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU ILI KULETA TIJA

**Na Mwandishi Wetu – Sumbawanga.**



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC wa Wilaya ya Kalambo. Wa tatu kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Bi Fatuma Muya na wa kwanza kutok kushoto ni Kaimu Katibi Msaidizi wa TSC Sumbawanga, Simon Simbujile.*

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Mbena Nkwama, ndc; amewataka Watumishi wa Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Sumbawanga, kufanya kazi kwa maarifa na juhudi kubwa katika kuwahudumia Walimu ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji elimu kwa wanafunzi ndani ya Manispaa ya Sumbawanga.

Aliyasema hayo hivi karibuni akizungumza na Watumishi wa Tume katika Wilaya hiyo akiwa katika ziara yake ya kawaida ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Majukumu ya Tume Wilayani iliyoendana na ushiriki wa Mafunzo ya Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS), yanayofanyika Wilayani hapo kwa siku nne kuanzia Machi 21 hadi 24, 2023 na kuhudhuriwa na Washitiri 24 kutoka Ofisi za Wilaya za TSC Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma huku pia yakiendelea katika vituo vingine viwili; Chuo cha Ualimu Korogwe chenye jumla ya Washiriki 30 kutoka Ofisi za TSC Wilaya zote za Mkoa wa Pwani na Tanga na kituo cha Bunda kinachojumuisha Mikoa ya Mara, Simiyu na Singida chenye jumla ya Washitiri 32 kufanya jumla ya Washitiri 86 kwa vituo vyote vitatu kwa ufadhili wa Wadau wa Maendeleo chini ya Mradi unaofadhiliwa na Program ya Shule Bora (SB).

Katibu huyo wa Tume Mwl. Nkwama alisema, "Mfumo huu mpya wa TEHAMA ujulikanao kama 'Teachers Service Commission Management Information System - TSCMIS' umejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha kazi ya kushughulikia mnyororo mzima wa Utumishi wa Walimu ikiwemo: Ajira za Walimu, Kuthibitisha Walimu Kazini, Kupandisha Walimu Vyeo, Kubadilisha Walimu Vyeo, Mirathi na Pensheni, Malalamiko ya Walimu, Usajili wa Wageni pamoja na kushughulikia Mashauri ya Nidhamu na Maendeleo ya Walimu."

Alisema kuwa TSC ni chombo cha kuwahudumia Walimu ambacho kimeundwa kwa mujibu wa Sheria Sura 448 na huduma hiyo hutolewa kwenye maeneo makuu matatu ambayo yanahusisha; Ajira ya Mwalimu, Maadili ya Mwalimu na Maendeleo ya Mwalimu kwa ujumla ikiwemo kuthibitishwa kazini, kuwapandisha vyeo, kuwabadilisha muundo baada ya kujiendeleza na mengine yote ya msingi katika Utumishi wa Mwalimu.

Aliongeza kuwa, Serikali kwa kutambua majukumu makubwa yanayotekelezwa na Tume ni wajibu wa watumishi wote kuzingatia weledi, kufanya kazi kwa bidii na kujituma huku juhudi na maarifa katika kumuhudumia Mwalimu vikizingatiwa.

Mwl.Nkwama alimshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuendeleza Sekta ya Elimu na sekta nyinginezo hapa nchini na kwa Taifa la Tanzania kwa ujumla wake katika kuleta maendeleo nchini.

Alisema kutokana na uongozi wake Walimu wamepandishwa madaraja na kubadilishiwa Muundo wa Utumishi, Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kusisitiza kuwa wajibu wa Watumishi hivi sasa ni kufanya kazi kwa juhudi, weledi, tija nakwa matokeo chanya ili Walimu wanaohudumiwa na Tume waendelee kuiamini na kuwatumikia wananchi inavyopaswa. Kila mmoja kwenye nafasi yake atimize wajibu wake.

Mfumo wa TSCMIS ulizinduliwa Machi 16, 2023 na Mhe.Angellah Jasmine Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akifungua Mkutano wa Pili wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na mfumo huo kuanza kutumika rasmi kwa ajili ya kushughulikia mnyororo mzima wa Utumishi wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini waliopo katika Utumishi wa Umma tukiendelea kuadhimisha Siku 730 za Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani.

# WATAALAMU WA MFUMO WA TSCMIS SIKU YA UZINDUZI WA MFUMO


















*Picha mbalimbali za wataalamu kutoka TSC walioandaa mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) wakati wa uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika Machi 16, 2023 katika Ukumbi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma.*

# KAMATI YA MABORESHO YA MITAALA YAENDELEA KUPOKEA MAONI KUTOKA KWENYE TAASISI MBALIMBALI ZA KIFEDHA

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es salaam.**



Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu wa kusimamia maboresho ya mitaala ya elimu ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu siku za karibuni ilipokea maoni na mapendekezo ya Viongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara hiyo juu ya kuingizwa masuala ya fedha katika mitaala ya elimu.

Kikao hicho kilifanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Jijini Dar es Salaam na kuongozwa na Mwenyekiti wa Kamati; Prof. Makenya Maboko, Wajumbe wa Kamati ya Maboresho ya Mitaala, Mkurugenzi Mkuu wa TET, Wajumbe kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Kitengo cha Fedha, Umoja wa Mabenki Tanzania, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Shirikisho la Asasi zinazotoa huduma ndogo za fedha.

# DKT. DUGANGE AIPONGEZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA KWA KUJENGA SHULE YA GHOROFA

**Na. Mwandishi Wetu – Arusha.**



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya Arusha kwa ubunifu wa kujenga majengo ya shule kwa kutumia michoro ya ghorofa katika Shule ya Sekondari Mpya ya Kiutu.

Dkt. Dugange alitoa pongezi hizo hivi karibuni wakati akikagua ujenzi wa shule hiyo mpya ya Kiutu inayojengwa kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Dkt. Dugange alisema kutokana na ufinyu wa eneo inapojengwa shule hiyo, Halmashauri iliamua kujenga baadhi ya majengo kwa mfumo wa ghorofa ambapo ili kutumia eneo hilo vema na aliridhishwa na hali ya ujenzi inayoendelea.

Alisema, "Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa shilingi milioni 470 za awali na Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani ilitoa shilingi milioni 250 ili kuwezesha ujenzi wa shule hiyo unaoendelea.

Aidha, Dkt. Dugange alieleza kuwa kutokana na makadirio ya awali bado zinahitajika shilingi milioni 111 ili kukamilisha ujenzi wa mradi huo ambapo makadirio ya gharama za ujenzi wa mradi huo zilikuwa shilingi milioni 696.

Kutokana na gharama za ujenzi na vifaa kupanda, aliiagiza Halmashauri hiyo kufanya tathmini ya mwisho ya kujua ni fedha kiasi gani zinahitajika kukamilisha ujenzi wa shule hiyo ili Uongozi uweze kutenga fedha za kukamilisha ujenzi.

Hali kadhalika, Mhe. Dkt. Dugange alimshukuru Diwani wa Kata ya Kiutu, Malaki Marambo na familia za jirani, kwa kutoa eneo la ujenzi wa shule hiyo kutokana na kata kukosa eneo la kujenga.

Shule ya Sekondari ya Kiutu tayari imepokea wanafunzi wa Kidato cha Kwanza 111 kati ya wanafunzi 133 waliokuwa wamepangwa kuanza masomo katika shule hiyo.

# WALIMU 17,000 KUPATIWA MAFUNZO KATIKA KUKUZA USTAWI WA MWANAFUNZI ILI KUWA NA DARASA SALAMA, SAIDIZI NA JUMUISHI

**Na. Mwandishi Wetu – Mikumi.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa kusirikiana na Shirika la Misaada ya Maendeleo la nchini Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Jifunze Uelewe wanatoa mafunzo kwa Walimu wa Shule za Msingi wanaofundisha Darasa la Kwanza hadi Darasa la Nne katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Ruvuma na Mtwara.

Mafunzo hayo yanalenga kukuza Ustawi wa Mwanafunzi katika kuwa Darasa Salama, Saidizi na Jumuishi yanafanyika katika Vituo vya Walimu (Teachers Resource Centre) nchini.

Katika kufanikisha zoezi hilo la utoaji wa mafunzo, TET kwa kushirikiana na USAID iliandaa Timu ya Wawezeshaji ya Kitaifa waliojumuisha Wakuza Mitaala wa TET na Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ambao walijengewa uwezo Wilayani Mikumi, Mkoani Morogoro mwezi Februari mwaka 2023.

Wawezeshaji hao waliendelea na jukumu la kuwaandaa wawezeshaji ngazi ya Mkoa na Wilaya ambayo waliwawezesha Maafisa Elimu ngazi ya Wilaya na Manispaa, Wadhibiti Ubora wa Shule na Walimu mahiri kwa mikoa ya Iringa, Mtwara, Morogoro na Ruvuma.

Baada ya mafunzo hayo viongozi hao walienda kuwawezesha Walimu mahiri katika ngazi ya Vituo vya Walimu ambao nao watawawezesha Walimu 17,000 kutoka Halmashauri zote za mikoa minne (Iringa, Mtwara, Morogoro na Ruvuma).



# TSC MBEYA YAWAJENGEA UWEZO WALIMU JUU YA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU









*Picha mbalimbali zikionesha mkutano kati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbeya na walimu ukiwa unaendelea. Mkutano huo ulilenga kuwajengea uwezo walimu juu ya kanuni za madili na utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na Wanafunzi Chuo cha Ualimu Sumbawanga (hawapo pichani) wakati alikutana nao hivi karibuni chuoni hapo.*

*Wanafunzi Chuo cha Ualimu Sumbawanga wakimsikiliza Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (hayupo pichani) wakati Katibu huyo alipofanya mkutano na wanafunzi hao hivi katika chuo hicho hivi karibuni.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga mara baada ya kufanya mkutano na wanafunzi hao chuoni hapo hivi karibuni.*





**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania